

LULU ŽA BUSARA KWA WAHIFADHI CHIPUKIZI

Ushauri kutoka kwa vizazi
vichache vya washindi wa
Tuzo za Whitley

Zana hii iliundwa kama
ushirikiano kati ya:



SUPPORTING
CONSERVATION
LEADERS



CONSERVATION
OPTIMISM

UTANGULIZI

Iwapo kuna wakati ambapo matumaini yanahitajika ni sasa. Kwetu sisi ambao tunajali mazingira, changamoto wakati mwingine zinaweza kuonekana kuwa nyingi zaidi. Ni rahisi sana kuhisi kama hatuna uwezo wa kukabiliana na upotevu wa viumbe hai, uchafuzi wa mazingira na mabadiliko ya hali ya hewa yanayoendelea - na mwendo wa pole wa viongozi wa dunia katika makubaliano ya sera za kushughulikia changamoto za kimataifa.

Hata hivyo, sababu za kuwa na matumaini zinatuzunguka mahali tulipo, katika kazi za kutia moyo za wahifadhi wa mazingira na jamii za wenyeji kote ulimwenguni ambao wanachukua hatua za ufanisi kulinda wanyamapori na mazingira. Ni wazo kuu la Whitley Fund for Nature kusaidia kazi ya mashujaa hawa wa uhifadhi wa mazingira na kuhakikisha wanapata kutambuliwa wanavyostahili. Uzoefu wa kila mshindi wa Tuzo la Whitley ni ya kipekee. Kwa pamoja ushindi wao unaonyesha kuwa - popote ulipo na vyovyote vile ambavyo changamoto zinaonekana kuwa kubwa - kazi ya uhifadhi inaweza kuleta mabadiliko. Kijitabu hiki kinatumia mambo waliokabiliana nayo ili kuonyesha jinsi inavyoweza kufanywa.

Ujuzi unaohitajika kwa hatua ya uhifadhi wa mazingira ulio na mafanikio si ule tuliojifunza shuleni. Na "kujifunza kwa kufanya" kunaweza kuonekana kuwa kungumu na kwenye upweke kwa mhifadhi wa mazingira mchanga aliye katika eneo la mbali kijijini na anayejitahidi kushughulikia shida ngumu na mara nyingi za dharura. Katika kijitabu hiki, watendaji ambao wamekuwa viongozi katika nyanja zao tofauti wanatueleza walichokisoma maishani mwao, wakitoa ushauri, msukumo, maneno ya kutia moyo kwa wale wanaoanza safari sawa.

Kwa maana hii, kama mseto wa hekima ya pamoja ya washindi wa Tuzo la Whitley kutoka duniani kote, kijitabu hiki kitumika kama mshauri kwa wataalamu wachanga wa taaluma. Maarifa yanyopatikana kwenye kila ukurasa sio "maelekezo ya mafanikio", kwani hakuna jambo kama hilo lililoko katika kazi ya uhifadhi. Badala yake yanaweza kutumika kama visaidizi vya kufanya maamuzi, na kama pembejeo za masomaji kuijendeleza katika mikakati yao ya mafanikio, kwa kuchukulia miktadha mahali wanakofanyia kazi.

Ninapendekeza kijitabu hiki kwa wahifadhi wa mazingira kila mahali, vijana kwa wazee, kama rasilimali muhimu ya kugawana na kujifunza - na kama chanzo cha matumaini kwa maisha yetu ya baadae.



Paula Kahumbu (Mkurugenzi Mkuu wa WildlifeDirect na mshindi wa Tuzo ya Dhahabu ya Whitley 2021)





YALIYOMO

Utangulizi	1
Muhtasari	3
Siri za ushirikiano mwema	5
Nguvu ya mawasiliano	8
Jinsi ya kufaulu katika usimamizi wa mradi	11
Kuongoza kwa huruma	14
Wakati mambo yanapokuwa magumu	17
Sanaa ya kuchangisha fedha	20
Vidokezo vya kuanza	23
Kutana na wachangiaji	25

UTANGULIZI

Tunaamini kwamba ulimwengu ambao watu na mazingira hustawi inawezekana. Lakini ili maono haya yatimie, tunahitaji watu wengi iwezekanavyo kujisikia kuwa wenye uwezo wa kutenda kama wahifadhi wa mazingira.

Zana hii inalenga kuwapa wahifadhi wa mazingira chipukizi vidokezo na kuwatia moyo wanaohitaji kuleta mabadiliko kwa mazingira. Ili kufanya hivyo, tulipata ujuzi na uzoefu wa washindi wa Tuzo za Whitley (Whitney Award) zinazoungwa mkono na Whitney Fund for Nature (WFN).

Shirika la hisani la Uingereza (UK Charity), WFN hutambua na kuunga mkono mashujaa wa mazingira walioko vijiji kutoka kote Ulimwenguni Kusini, ambao wanatekeleza miradi ya hivi punde ya kisayansi na kuongoza miradi ya mashinani kwa ari. Wote wanaleta manufaa yanayoonekana kwa viumbe wa porini, mandhari na watu. Mafanikio yao ni chanzo kizuri cha msukumo kwa wahifadhi wa mazingira wachanga kazini.

Ili kuunda zana hii na kuifanya iwe ya kuchangamsha tuliwahoji washindi 13 wa Tuzo la Whitley na kuwa uliwa watueleze kuhusu maeneo sita muhimu: ushirikiano, mawasiliano, usimamizi wa miradi, uongozi, ustawi na ustahimilivu, na uchangishaji fedha. Walizama kwa kina katika yale ambayo wameyapitia katika taaluma zao zote, bila kukwepa mada ngumu, na kutoa maelezo ya kuridhisha na kupendeza kweli.

Conservation Optimism imeundwa kwa imani kwamba kulinda ulimwengu wa kesho kunategemea watu wengi iwezekanavyo duniani. Kote wote wakijitokeza kuchukua hatua kwa ajili ya mazingira.

Kuwapa watu vidokezo kuhusu jinsi ya kuanza uhifadhi wa mazingira ni sehemu muhimu katika kufikia imani hii na ni jambo linalohusiana na Whitney Fund for Nature. Tunatumai kuwa utapata zana hii kuwa muhimu na kwamba utafurahia ushirikiano huu.

Imekuwa tukio la ajabu kwa timu zetu zote mbili kufanya kazi pamoja na tumependezwa na kina cha majibu tuliyopokea kutoka kwa washindi wa Tuzo za Whitley.

Mimi wako mwaminifu,

Julia Migné (Mkurugenzi wa Conservation Optimism) & Danni Parks (Mkurugenzi wa Whitley Fund for Nature)



MUHTASARI

Je, inawezekana kuwa huna muda wa kusoma zana nzima? Usiogope, tumekuletea ushauri muhimu kutoka kwa jopo letu la washindi wa Tuzo la Whitley hapa chini!

SIRI ZA USHIRIKIANO MZURI

1. Tambua washirika watarajiwa, ndani na nje ya sekta
2. Jiweke katika viatu vyao
3. Uwe mwenye kubadilisha msimamo na uzoefu wa haraka
4. Anzisha kuheshimiana na kuelewana
5. Kuza uaminifu kupitia mahusiano ya muda mrefu

NGUVU YA MAWASILIANO

1. Fanya ujumbe wako rahisi
2. Wakumbushe watu urembo wa mazingira
3. Tafuta njia mwafaka ya kuungana na watu
4. Weka ujumbe wako kulingana na hadhira unayolenga
5. Kuwa na shauku na matumaini

JINSI YA KUDHIBITI MRADI

1. Tambua unacholeta kwenye meza
2. Weka malengo yanayowezekana
3. Jifunze kutokana na kushindwa
4. Jipachike katika muktadha wa kijiji mwenu
5. Jenga timu imara

KUONGOZA KWA HURUMA

1. Sikiliza watu wanaokuzunguka
2. Kuwa mkarimu na mwenye shauku
3. Soma umati na upange uongozi kulingana na mahitaji yao
4. Washike mkono viongozi wanawake
5. Kuwa mnyenyeketu na wengine waangaze

WAKATI MAMBO YANAPOKUWA MAGUMU

1. Jenga mtandao wa usaidizi
2. Chukua likizo mara kwa mara
3. Jitie matumaini
4. Tumia muda wako katika mazingira
5. Angalia mbele katika malengo unayotaka kufikia

SANAA YA KUCHANGISHA PESA

1. Kuwa mwenye kushirikisha
2. Tambua jinsi bora ya kuuza mradi wako
3. Elewa wafadhili wako wanataka nini
4. Jenga uhusiano na wafadhili wako
5. Kuwa na uzoefu wa haraka

VIDOKEZO VYA KUANZA

1. Fanya mabadiliko katika maisha yako mwenyewe
2. Jifunze kupitia majoribio na makosa
3. Unda niche yako
4. Anza katika kijiji chako
5. Jifunze kutoka kwa taaluma zingine



SIRI ZA USHIRIKIANO MZURI

Kushirikiana na wadau mbalimbali ni muhimu kwa uhifadhi. Lakini ni nini hasa kinachohitajika ili kujenga ushirikiano wenyewe mafanikio? Na unapaswa kushirikiana na nani? Jopo letu la washindi wa Tuzo la Whitley ilikuwa na mawazo mengi kuhusu mada hii. Soma kwa mapendekezo yao!



“Jenga mtandao wa kushirikiana na usifanye kazi peke yako. Kuna mambo mengi ya kujifunza kutoka kwa watu wengine, haswa kutoka kwa watu wasiokuwa katika nyanja yako ya karibu. Na pia bila shaka fanya kazi na watu ambao sio wataalamu wa uhifadhi. Mojawapo ya furaha kubwa ya kufanya kazi katika sekta hii ni kubadili watu wapya wawe wahifadhi!”

- Rodrigo Medellín

Njia moja ya kufanya hivyo kulingana na Rodrigo, mhifadhi popo anayefanya kazi nchini Mexico, ni kujihusisha na mambo yanayoendelea tunakoishi “kamwe usiache kufanya eneo lako la faraja kukua”. Lakini ni muhimu kutambua ni nani unapaswa kufanya kazi naye kabla ya kuanza kujenga mtandao huo.

Hotlin Ompusunggu, Daktari wa Meno ambaye alihamia Sumatra mwaka 2019 na kuanzisha Shirika lisilo la kiserikali la Healthy Planet Indonesia (HePI) kwa msaada wa WFN Continuation Funding, anatuambia kuwa ushirikiano bora ambao amekuwa nao katika kazi yake kama mhifadhi ni pamoja na jamii zinazoishi kando ya misitu ya mvua. “Mambo bora zaidi niliyokabiliana nayo ni ushirikiano tunaposikilizana na kuheshimiana na kutendeana kwa utu na kuthaminiana, uaminifu, na uwazi”. Marleny Rosales-Meda, ambaye anafanya kazi kuhusu matumizi bora ya misitu nchini Guatemala, anakubaliana juu ya umuhimu wa kufanya kazi na wenyiji na anaongeza kuwa “ni muhimu kwa watu wanaohusika katika mradi wako kujisikia kuthaminiwa na kujua kwamba mchango wao unathaminiwa”.

Kwa Dino J. Martins, mtaalam wa wadudu wa Kenya, ilikuwa muhimu kuwasiliana na wakulima kama sehemu ya lengo lake la kuboresha ufahamu wa wadudu na uhifadhi. Anaeleza: “Jambo nililojifunza mapema kutoka kwa mama yangu ni kwamba unakamata nzi wengi kwa asali kuliko kwa siki. Kwa hiyo, falsafa ambayo nimeikubali maishani ni kwamba ni rahisi kufanya kazi na watu unapowasikiliza, unapowaheshimu, unapoelewa.”

Dino anaamini sana uwezo wa kustaajabisha na mara nyingi huwaonyesha wakulima wadudu kama vile vidukari (“shetani aliyefanyika mwili kwa mkulima”) kupitia hadubini na akasema kwamba “wanapeperushwa tu na wakastaajabu” kwa kuwaona viumbe vidogo karibu. Hilo ndilo jambo ambalo Pablo Borboroglu, mhifadhi wa pengwini anayefanya kazi nchini Ajentina, anaweza kuhusiana nalo: “Uhifadhi una vipengele vingi tofauti. Sio kazi ya kawaida tu kwa hivyo ni muhimu sana kuanzisha uhusiano wa kihemko na watu katika timu yako na jamii vijijini.



Dino J. Martins akisambaza furaha ya wadudu na wakulima nchini Kenya

Hata hivyo, kumbuka kwamba kujenga uhusiano na watu, bila kujali wao ni nani, inachukua muda na jitihada. Laury Cullen hufanya kazi nyingi na jumuiya katika Msitu wa Atlantiki ya Brazili na anaeleza: “Mengi tunayofanya yanahuisha jamii vijijini na yanahuiana na kiburi na uaminifu. Unapopata timu moja inayofanya kazi na wenyiji sawa katika biashara moja kwa muda mrefu basi unapata uaminifu, unakuza uhusiano. Kwa hivyo ningependekeza kuwa uwepo wa muda mrefu ni muhimu ikiwa unataka kujenga uaminifu na kiburi na jamii za wenyiji.





Shivani Bhalla, ambaye anakuza uhusiano wa binadamu na wanyama wala nyama nchini Kenya, anakubaliana na ukweli kwamba ushirikiano huchukua muda kutekelezwa lakini pia anaongeza kuwa ni muhimu kujua wakati wa kukatiza uhusiano ambao haujafaulu. "Jambo la msingi kwa ushirikiano ni kwamba inachukua muda kuibaini. Usikimbile kuingia katika ushirikiano. Na ushirikiano mwengine hautafanikiwa kwa hivyo usiogope kusema: samahani, huu haufanyi kazi na tunahitaji kuendelea.



Laury Cullen kwenye kitalu cha miti ya jamii nchini Brazili

Kiungo cha mwisho cha ushirikiano wenye mafanikio? Caleb Ofori-Boateng, mtafiti katika masomo ya reptilia na amfibia wa kwanza aliyefunzwa rasmi nchini Ghana, anatukumbusha kwamba ni muhimu kukumbuka kwamba si kila mtu anafikiri kama sisi, "watu waamotisha tofauti na watu wana sababu tofauti za kujihusisha au la". Kwa hivyo kujiweka katika viatu vya watu wengine kunaweza kutusaidia kupata ufahamu bora wa maeneo tunayofanya kazi. Ili kufanya hivyo, tunahitaji kuwa na uwezo wa kubadilisha msimamo na kubadilika. "Lazima ufanye kazi na wengine na lazima uwe wazi kila wakati kwa mawazo mapya au njia za kufanya mambo", anasema Gladys Kalema-Zikusoka, mhifadhi anayelinda sokwe nchini Uganda. "Nadhani ni moja wapo ya uwanja ambao unapaswa kuwa na uwezo wa kubadilika sana. Hauwezi kuwa mgumu sana wa mabadiliko kwani hautafikia malengo yako."

"Uhifadhi unahuwa watu kwa hivyo tunapaswa kuwaunganisha. Unapokuwa dhabiti na sugu watu huwa wanakusikiliza."

- Purnima Barman



NGUVU YA MAWASILIANO

Kutambua wadau wako ni hatua muhimu lakini utawezaje kuwasilisha malengo yako kwa wasikilizaji hao? Washindi wa Tuzo za Whitley wamelazimika kuwa watalam katika mawasiliano, ili kuongezana kuihua mafanikio yao na kubuni miradi yao. Wanatafakari juu ya mambo au hatua ambazo zimekuwa za manufaa kwao na kutueleza vidokezo vifuatavyo.

"Kwa kweli natamani ningewasiliana zaidi ili mawasiliano, mawasiliano, mawasiliano! Usizingatie maelezo ya kindani, hayajalishi ikiwa ni mawasiliano ya umma. Lakini ni muhimu sana uende kwa kujiamini!" - Amanda Vincent



Marleny Rosales-Meda anaangazia umuhimu wa mawasiliano kwa kuongeza kuwa kama wahifadhi "tunahitaji kujifunza njia mpya ya kuwasiliana ili kuwa wawasilianaji wenye ufanisi". Anaamini kwamba hii itaturuhusu kupata ujumbe wa wazi kutoka kwa watazamaji wetu na kuhamasisha watu kuchukua hatua kwa ajili ya mazingira.



Vijana wa Maya-Q'eqchi' wakifurahia kujifunza kuhusu kilimo cha permaculture na upandaji miti upya wakati wa warsha ya matumizi ya mafunzo

Amanda Vincent, mwanabiolojia wa baharini anayefanya kazi Ufilipino, ana sheria zake tatu za mawasiliano: jua ujumbe wako, jua hadhira yako, na uuweke rahisi. Sehemu ya kujua watazamaji wako inahusiana haswa na Elena Bykova, mtaalamu wa mamalia kutoka Uzbekistan, kwani anaamini kuwa ni muhimu kuwasiliana na watu katika viwango vyote vya jamii. Anaeleza kuwa "unahitaji kuwa na lugha sawa na kila mtu unayefanya naye kazi, ikiwa ni pamoja na wenyeji wanaoishi katika maeneo ambayo unataka kulinda".





Wakati mwingine ni muhimu kukumbuka pia kwamba kuonyesha watu jinsi asili ilivyo nzuri inaweza kuwa njia yenyeye nguvu ya kuwashirikisha katika uhifadhi. Tuna jumbe nyingi nzito tunazotaka kushiriki kuhusu kazi tunayofanya lakini Dino J. Martins anatukumbusha kuwa kuunganisha watu na uzuri wa asili wa viumbe tunaofanya kazi ni njia nzuri ya kujenga madaraja. "Jambo gumu zaidi kufanya kazi na wadudu ni kwamba watu wengi wanawaogopa.

Jinsi ninavyofanya kazi ya kuwaunganisha watu na wadudu ni kwa kuwaonyesha maumbo na rangi zao", asema. "Kuwafanya kukaa kimya na kutazama na kusikiliza na kutazama. Na ninaona hiyo ni njia yenyeye nguvu sana kwa watu kutambua kwamba hapa kuna kiumbe huyu mdogo ambaye anaonekana mgeni sana na bado anafanana sana na sisi!"



Hili ni jambo ambalo Amanda anaweza kulihusisha huku akieleza kuwa changamoto yake kubwa ni kwamba samaki mara nyingi hawachukuliwi na watu kama wanyamapori. "Bado ni changamoto kubwa kueleza watu kwamba samaki ni wa porini na kwamba wanastahili heshima na kuungwa mkono na uhifadhi", anaongeza. Aligundua kuwa spishi anazozingatia zaidi, farasi wa baharini, wamemsaidia kuvunja vizuizi vingi. Anasema: "Nafikiri mojawapo ya hatua za hekima zaidi tulizofanya ni kutayarisha samaki wa baharini. Unazungumza juu ya farasi wa baharini na unahisi uhusiano na heshima fulani kutoka kwa watu. Ni wazuri peke yao lakini pia walifungua milango kwa wingi wa samaki wengine wa baharini". Kuwa na mkakati kuhusu jinsi unavyopanga kazi yako kunaweza kuleta mabadiliko makubwa katika jinsi mawasiliano yako yanavyoweza kupokelewa!

Kuweka ujumbe wetu kwa njia tofauti ili kufikia hadhira tunayotaka kufikia ni sehemu nyingine muhimu ya mlinganyo. Kama sehemu ya kazi yake ya kulinda swala aina ya saiga Elena Bykova anajihuisha na jumuiya mbalimbali za wenyeji na anaeleza kuwa "kwa kurudi mara kwa mara na kuunganisha saiga na mifumo yao ya kihistoria na kiroho walianza kupendezwa". Anasema: "Hاتua iliyofuata ilikuwa kuwaonyesha kwamba wakati ujao wa saiga hautegemei watafiti kutoka nje lakini kwamba wanaweza kuwa na athari ya moja kwa moja katika kulinda viumbe. Kwa hivyo tunawahimiza kuangalia tabia zao wenyewe na kufikiria juu ya athari ambayo ujangili wa spishi unapata.

Wadau mbalimbali wana njia tofauti tofauti za kuwasiliana kwa hivyo ni muhimu kuzingatia hilo. "Kama tungekuwa tunafanya kazi, tuseme na serikali, hawataki kusoma ripoti za utafiti mrefu," anaelezea Gladys Kalema-Zikusoka. "Hawatawahi kuzisoma, wanataka tu kitu kifupi sana. Kwa hivyo ikiwa umefanya utafiti na kuna kitu kutoka kwa utafiti ambacho ungependa serikali ifuatilie, lazima uwape muhtasari wa utafiti huo. Rodrigo Medellín pia anaangazia uwezo wa kupanua mitazamo yetu ili "kufikia watoa maamuzi, wamiliki wa ardhi, watoto, na vikundi vingine vyovypote vya watu ambao wameunganishwa na masuala ambayo unashughulikia".

Tunajua kwamba tunahitaji kushirikisha hadhira tofauti katika uhifadhi lakini ni jinsi gani tunawawezesha watu kuchukua hatua na kuleta mabadiliko kwa sayari hii? Caleb Ofori-Boateng anaamini kuwa mengi yanahusiana na matumaini. Anasema: "Shiriki upande wenye matumaini wa mambo. Kuwa na mtazamo mzuri. Tambua kuwa watu huchagua jema badala ya uovu kwa hivyo wauze maono ya siku zijazo na kuunda masuluuhisho au hatua zinazofuata ili kusaidia kutambua wakati ujao."

*"Huna haja ya kuzungumza sayansi,
unahitaji kuzungumza mapenzi. Yote ni jinsi
inavyowafanya watu wahisi!"*
- Pablo Borboroglu





JINSI YA KUDHIBITI MRADI

Kufanya kazi katika uhifadhi mara nyingi huhusisha kiasi fulani cha usimamizi wa mradi. Lakini ni nini hufanya mradi wenyewe mafanikio? Na tunaweza kuziongeza ili kuongeza athari zetu? Hilo ni jambo ambalo washindi wote wa Tuzo la Whitley wamelazimika kuliboresha taaluma zao ili wawe na mapendelekezo mengi kwa ajili yetu!



“Ni muhimu kujijua mwenyewe na nini unaweza kuwekeza katika uhifadhi. Sote tuna ujuzi tofauti, uwezo wa kimwili, uzoefu wa maisha, na uzoefu wa kitaaluma kwa hivyo fikiria juu ya jambo unaloweza kuleta uwanjani na ni njia gani bora kwako ya kuchangia.”
- Elena Bykova

Moja ya mambo ya kwanza kabisa tunayopaswa kufanya wakati wa kusimamia miradi ni kurekebisha malengo yetu. Inajaribu kurekebisha malengo kabambe ambayo yatatuleta karibu na athari tunayotarajia kuwa nayo. Hata hivyo, Caleb Ofori-Boateng anapendekeza kwamba “ni bora kuweka malengo ya kweli ili kuleta athari na kuruhusu athari hiyo ikubebe kwenye hatua yako muhimu”.

Pablo Borboroglu pia anaamini kwa dhati umuhimu wa kuwa wa kweli na anaongeza: “Ni muhimu sana kuwa na utambuzi mzuri wa tatizo tangu mwanzo kabisa. Kisha unaweza kupata suluhisho zenye manufaa.” Anasisitiza kwamba kuruka hatua hii kunaweza kusababisha kuwekeza muda mwangi, pesa, na nishati katika suluhisho ambalo halitawahi kubadilishwa kulingana na muktadha.

“Kumbuka tu lengo lako,” asema Pablo. “Kutakuwa na dhoruba nyingi, kutakuwa na nyakati nyingi ambapo unasema: ‘Loo, sijafaa kwa hili au sikuwa mtu sahihi kwa hilo’. Lakini dhoruba hutokea na ni vyema kwa wahifadhi kuwa marubani wa dhoruba.”



Uhifadhi ni kweli mara nyingi kuhusu kucheza mchezo mrefu na kustahimili dhoruba. Elena Bykova anaeleza kwamba: “Uhifadhi si tu kuchukua hatua kwa siku moja au mwezi mmoja. Ni jambo la kudumu kwa hivyo unapaswa kuwa tayari kwa hili na unahitaji kuelewa jukumu lako tangu mwanzo.

Lakini ingawa tunahitaji kuweka macho yetu kwenye upeo wa macho, ni muhimu pia kuchukua muda kujipachika wenyewe katika muktadha wa ndani na kuelewa asili ya kitamaduni na kiroho. Marleny Rosales-Meda anaelezea kuwa hii “inaweza kusaidia sana na itakuruhusu kuunda rasilimali pamoja na jumuiya za wenyeji, ambayo inaweza kuwa na nguvu zaidi”.

Jambo jingine muhimu kwa usimamizi mzuri wa mradi ambalo washindi wengi wa Tuzo la Whitley walikubali ni kujenga timu imara. Ingawa Elena anaangazia umuhimu wa kuwaleta pamoja washiriki wa timu mbalimbali lakini wanaokamilishana, Caleb anakumbuka kwamba alikuwa akifikiri angeweza kufanya kila kitu peke yake alipokuwa mdogo lakini akagundua: “Kuweza kuleta matokeo na kuiga chochote ninachowea kufanya. nikifanya, nahitaji kuzingatia kujenga uwezo”.

Pablo anaongeza: “Ikiwa utasimamia mradi mkubwa, ni muhimu kujua mapungufu yako na kuajiri watu. Waajiri wanasheria, waajiri watanunza hesabu, waajiri wanasaikolojia, yeyote unayehitaji katika timu yako. Kuwa na muundo mdogo unaopanuka na mikataba kulingana na mahitaji ya miradi humpa yeye na timu yake unyumbu wanaohitaji kuzoea haraka.



Kuwa na watu wa kujitolea wanaotusaidia kufikia malengo yetu pia ni njia nzuri ya kuongeza matokeo huku tukiwapa watu njia ya kuleta mabadiliko kwa ulimwengu. Hata hivyo, profesa wa uhifadhi wa Kituruki Çağan Sekercioğlu, anaangazia kuwa ingawa “kuwa na watu wazuri wanaojitolea kutaongeza matokeo yako, unapaswa kuchagua watu wako wa kujitolea kama vile unavyochagua wafanyakazi” na kuwa na mchakato murwa wa kuchagua.

Kuzoea upesi mara nyingi ni muhimu katika uhifadhi na kwa hivyo kujifunza kutokana na kutofaulu ni muhimu sana kuweza kurejea mambo yanapoenda kombo. Amanda Vincent aeleza hivi: “Ikiwa utaweza kushinikiza zaidi a hatua fulani, utakosea mara kwa mara.” Kidokezo kimoja muhimu alichojifunza kutokana na kutofaulu ni kwamba “huwezi kukimbia ikiwa kuna vizuizi vingi sana kwenye njia yako, lazima uchague njia yako kwa uangalifu”. Anaongeza kuwa kuamini timu yako pia ni sehemu muhimu ya kusimamia miradi.

Akiwa mhifadhi simba, Shivani Bhalla alilazimika kubadilika na kunyumbulika katika maisha yake yote. Anasema: “Uhifadhi hubadilika sana na vitisho vinabadiika sana. Nikiangalia vitisho vya miaka 15 iliyopita kwa simba na nikiangalia vitisho kwao sasa, baadhi ya vitisho vya zamani sio vitisho tena lakini kuna vitisho vipyta vinavyoibuka na huwezi kukwama katika njia zako za zamani. Unapaswa kuzoea, kubadilika na kuzingatia vitisho vipyta na ujaribu kushughulikia ikiwa una uwezo wa kufanya hivyo.

Wakati mwingine inaweza kuwa ngumu kujua ni mwelekeo gani wa kupanua wakati miradi inakua lakini ni muhimu kutoruhusu hilo litulemaze. “Nafikiri wahifadhi wengi, hasa wale walio katika taaluma, wanatasita kuendelea kwa sababu wangependa kujiamini zaidi,” anaeleza Amanda. “Lakini ukweli ni kwamba kila wakati tunayo habari ya kutosha kufanya aina fulani ya hatua katika mwelekeo sahihi.” Kwa hivyo hatuna budi kuendelea na kama Purnima Barman, mhifadhi anayelinda korongo wakubwa zaidi nchini India, asemavyo: “Lazima tulete nguvu na shaku. Tunapaswa kuhangaika!”.

“Katika uhifadhi lazima ufikirie nje ya sanduku kwa sababu uhifadhi sio tu juu ya wanyama au misitu, ni juu ya watu.”
- Gladys Kalema-Zikusoka



KUONGOZA KWA HURUMA

Washindi wa Tuzo la Whitley walioangaziwa katika zana hii wote wanatambuliwa kama viongozi katika nyanja zao. Lakini ni nini kinachohitajika ili Kuongoza timu kwa uangalifu? Wanashiriki ushauri wao kwa viongozi wa uhifadhi wa siku zijazo.

.....
: “Unapoweka shauku katika kile unachofanya, unapopenda kazi yako, unapopenda sana aina yako au eneo lako au chochote unachofanya kazi, watu wanaona hivyo na timu yako inaona hivyo. Na kisha inaambukiza. Wanapata nishati hiyo na wanataka kuwa mali.” - Pablo Borboroglu
.....



Kuongoza ni juu ya kuwasikiliza watu na si lazima kuwa mchakato wa ngazi ya juu. Hotlin Ompusunggu anaeleza kuwa anampa kila mtu fursa ya kuongoza anapofanya kazi na jumuiya za wenyeji. Anaongeza: “Tunapofanya mikutano na jumuiya tunazungusha gurudumu kuamua nani ataongoza mkutano. Kwa hiyo mtu huyo anaweza kuwa mpishi au dereva au kuwa na kazi nyingine yoyote na bado akapata fursa ya kuongoza mkutano.”





Kupitia mazoezi haya anajenga utamaduni fulani wa kazi na kuhakikisha kwamba kila mtu anahisi kusikilizwa. "Inaonyesha tunawaheshimu na tunawasikiliza. Na kila wakati tunapokutana tunafanya mduara, ili hakuna mtu ambaye ni mwenyekiti wa mkutano. Kila mtu ana mwingiliano sawa na sisi na hakuna mtu nyuma ya mtu mwingine. Tunajaribu sana kupata muundo huo wa kijamii ili kupata kila mtu kuthaminiwa sawa na kwa kila mtu kuwa na fursa sawa ya kushirikiana na wengine.

Amanda Vincent anakubaliana na hoja za Hotlin na anaamini kwamba tunaweza kufanya maendeleo tu wakati tunatambua mahitaji ya watu. Ni muhimu kusikiliza timu zetu na kutathmini kile wanaweza kuhitaji kutoka kwetu. Kwa Amanda, viungo vinavyohitajika kuongoza ni shauku, uthubutu, na "dollop nzito ya wema".



Shivani Bhalla akiwa na wanawake wenyeji nchini Kenya

Kusoma umati na kurekebisha jinsi tunavyoongoza ni jambo lingine ambalo washindi wengi wa Tuzo la Whitley walonyesha. Çağan Sekercioğlu anaeleza kuwa kusikiliza watu ndio jambo la muhimu kwake kufanya kama kiongozi. Anaongeza: "Watu wengine wanaweza kuogopa kuzungumza na bosi ili iwe na manufaa kuwavuta kando na kuwaliza mara kwa mara jinsi wanaendelea". Marleny Rosales-Meda alilazimika kujifunza kuwa kiongozi kama msichana anayefanya kazi kimsingi na wanaume. Anaeleza kuwa anakofanya kazi Guatemala "wanaume huwa na maamuzi na wanawake wanaweza kuonekana dhaifu" kwa hivyo ilichukua mengi kwa watu kumwamini. Lakini anaamini sana kuwa wanawake wana kitu cha kipekee cha kuleta katika nafasi za uongozi. Anasema: "Kama wanawake tuna maono ambayo ni ya kipekee, ya muda mrefu na yenye kina zaidi. Tunaelekea kuwa na huruma zaidi na tuna uwezo wa kutatua migogoro na kufanya kazi kwa vikundi".

Shivani Bhalla pia anatoa wito kwa viongozi wanawake zaidi na ana ujumbe muhimu, hasa kwa wale wanaofanya kazi barani Afrika. "Ikiwa wewe ni mwanaume katika nafasi ya madaraka, kuwa na huruma kwa wanawake! Kuna viongozi wa uhifadhi barani Afrika ambao hawapewi nafasi za kuwa viongozi au kupanda katika viwango. Chini ya 5% ya viongozi wa uhifadhi barani Afrika ni wanawake na hilo lazima libadilike. Wanawake wanahitaji kuanza kupitia vizuizi hivi nya kichaa ambavyo tunaendelea kukumbana navyo, lakini wanaume wanahitaji kuunga mkono sana hilo. Anaongeza kuwa utofauti ni muhimu sana katika timu na ni jambo ambalo viongozi wanahitaji kuangalia. "Lazima tuenze kuzingatia na kuwapa kipaumbele viongozi ambao wanatoka Afrika na sio mtu anayekuja kutoka nje na kutuambia la kufanya."

Rodrigo Medellín anaongeza kuwa kipengele kingine muhimu cha kuwa kiongozi ni kuweka chaguo zetu wazi iwezekanavyo na kutomtupilia mbali mtu yeyote. Hatujui ni nani anaweza kuwa mshirika wa siku zijazo au ambaye anaweza kuleta ujuzi ambao hatukutambua tulikuwa nao ndani ya timu zetu.

Lakini je, tunawavutiaje wenzetu? Elena Bykova anaamini kuwa upendo ndio msingi wa ujenzi. Anasema: "Upendo ni muhimu sana! Unahitaji kupenda unachofanya na kupenda aina yako au eneo ambalo unafanya kazi ili kuwatia moyo watu wengine". Amanda anaongeza kuwa kuweka hali ya matumaini katika timu yetu ni muhimu.

Sehemu ya mwisho ya fumbo kulingana na Shivani pia ni kuwa mnyenyekemu na kuwapa washiriki wa timu fursa ya kung'aa kila inapowezekana. "Hii sio juu ya ubinafsi wetu, hii inahusu timu zetu. Na nadhani tunashindwa sana katika uhifadhi ambapo una mfano huu wa uso mmoja. Una shujaa huyu mmoja, anayeongoza timu na hiyo sio endelevu. Kwa hivyo tunahitaji kuhakikisha kuwa timu zetu zinapata sifa zinazostahili na uwezekano wa kuwa sura ya miradi wanayosimamia.

"Unapaswa kudhahirisha hali ya furaha, shauku, msisimko, na matumaini kadiri uwezavyo. Na kisha hakikisha kuwa timu inahisi maendeleo na mafanikio."

- Amanda Vincent





MAMBO YANAPOKUWA MAGUMU

Kama wahifadhi tunakabiliana na matukio ya kutisha kama vile makazi kuharibiwa, au spishi zinazotoweza. Inaweza kuwa ngumu kuendelea. Kwa hivyo ni mbinu gani ambazo washindi wa Tuzo za Whitley hutumia wakati kazi ya uhifadhi inakuwa ngumu?



“Wahifadhi wanaifanya dunia huduma. Spishi moja baada ya nyingine, mti mmoja kwa wakati, tunaifanya dunia kuwa mahali pazuri zaidi kwa wanadamu wote. Watu wanapaswa kutambua jukumu la wahifadhi kwa ajili ya maisha yetu ya baadaye na kutuunga mkono kwa njia yoyote ile. Katika lahaja yangu ya kienyeji, tuna methali muhimu. Inamaanisha, ‘ikiwa huniungi mkono, angalau usifanye mambo kuwa magumu kwangu.” - Caleb Ofori-Boateng

Kitu ambacho kila mtu anakubaliana nacho ni hitaji la kutanguliza afya yetu ya kiakili na kimwili. Hotlin Ompusungu anaeleza kwamba ye ye hujitahidi kuwa na mawasiliano ya mara kwa mara na marafiki na wanafamilia wake. Anasema: “Ni vizuri kuwasiliana sikuzote na familia yako na marafiki lakini hupaswi kushiriki tu mafanikio yako na unapaswa kushiriki matatizo yako pia!”. Anaongeza kuwa pia anajali afya yake kwa ujumla kwa kuzingatia kile anachokula, kufanya mazoezi mara kwa mara na kupata usingizi wa kutosha.

Shivani Bhalla pia amejifunza katika maisha yake yote jinsi ilivyo muhimu kwake kutilia maanani ustawi wake. Anaongeza: “Unapoishi na kufanya kazi mahali pamoja, ni muhimu sana kurudi nyuma na kutanguliza afya yako. Ikiwa hutafanya hivyo, ghafla unakumbwa na masuala ya afya. Kwa hivyo fanya ustawi kuwa sehemu ya maisha yako ya kila siku!”. Sasa ameingia katika mzunguko wa kuchukua likizo kila baada ya wiki sita.

Anaeleza: “Hilo limekuwa badiliko kwangu! Ninaacha kabisa kila kitu na ninaifanya kuwa sehemu ya ahadi zangu. Ninapanga wakati huo katika miezi yangu ya kalenda mapema na kuiambia timu yangu kuwa hakuna kitu kinachofanyika kwangu kwa siku 10 zijazo. Na hilo limesaidia sana ustawi wangu”. Kuhakikisha anaenda kwa madaktari anapojisikia vibaya na kuonana na mtaalamu wa akili mara kwa mara ni mambo mengine ambayo Shivani huona kuwa ya manufaa.

Wengine hupata kitulizo kwa kuwa na matumaini kuhusu wakati ujao. Rodrigo Medellín anasadiki kwamba hatuwezi kukimbia hatari ya kuwa na tamaa. Anaeleza hivi: “Tayari dunia ni mahali pa kusikitisha sana na nimetambua kwamba ikiwa nitakuwa mtabiri, mwenye kukata tamaa, nitaharibu urithi wangu. Kwa hivyo ninajaribu kutia moyo matumaini kadiri niwezavyo katika vizazi vichanga na ninawawezesha vijana wengi kadiri niwezavyo. Nataka wawe viongozi wao wenyewe popote walipo”. Amanda Vincent pia anaamini kwamba kubaki na matumaini ni muhimu kwake kuendelea.



Caleb Ofori-Boateng akipata furaha uwanjani nchini Ghana

Anasema: “Siku zote kuna njia ya kusonga mbele. Wakati fulani inabidi ufanye bidii kuitafuta lakini ikiwa uko tayari kugeuza ubongo wako na kuchunguza mawazo tofauti basi kutakuwa na kitu ambacho unaweza kufanya ambacho ni muhimu na chenye manufaa.” Gladys Kalema-Zikusoka pia anapenda kusherehekeea ushindi na mafanikio kila yanapotokea na anaeleza kuwa inampa motisha ya kusonga mbele zaidi.

Dino J. Martins pia anasisitiza umuhimu wa kuwa na matumaini kuhusu siku zijazo. Anatutia moyo tuwe na tumaini hata wakati inaonekana hakuna tumaini na anakazia umuhimu wa kutumia wakati kuhusiana na mazingira. Anaongeza kuwa kufanya hivyo “kutakuwa chanzo cha lishe katika nyakati hizo ngumu sana”.



Kutumia muda katika maumbile ndiko kulikotufanya wengi wetu kuwa wahifadhi. Ni jambo ambalo tunalipenda na kufurahia kufanya. Caleb Ofori-Boateng anatukumbusha kuzingatia kile ambacho matamanio yetu ni kweli. Anasema: "Kufanya kazi katika uhifadhi kuna changamoto nyingi na kunahitaji kujitolea mhanga. Na kutokana na ujuzi wangu, sababu ambayo imeniwezesha kuendelea ni kwa sababu ninamsukumo wa kindani. Nina shauku sana juu ya kile ninachofanya."

Tukiangalia mbele kwa malengo tunayotaka kutimiza ni mkakati mwengine wa kuzidi kuendelea wakati mambo yanapokuwa magumu. Laury Cullen na timu yake wana kile wanachokiita Ramani ya Ndoto. Anaeleza: "Ramani hiyo ni kama bosi wetu! Tuna ndoto na tunajua tunakotaka kufika. Tunaangalia ramani hiyo na tunaona furaha mwishoni! Na tunaona kwamba wanaotuunga mkono wana nia ya kweli kutusaidia na misheni yetu ya muda mrefu." Kamwe usidharau nguvu ya kuwa na watu wanaotuunga mkono na kutushangilia pia!



"Tunaona matokeo ya jitihada letu, shauku, na upendo kwa kile tunachofanya kila siku. Huo ni msukumo mzuri sana."
- Laury Cullen



SANAA YA KUCHANGISHA FEDHA

Kwa hivyo sasa tunajua zaidi kuhusu kile kinachomfanya kiongozi awe mwenye huruma, jinsi ya kuwasiliana na kushirikiana na wengine, na jinsi ya kutunza afya yetu ya kiakili. Lakini bado tunakosa kipengele muhimu cha kufanya kazi katika uhifadhi: kuchangisha pesa. Siku hizi, kuweza kuchangisha fedha kwa ajili ya miradi ni sehemu muhimu ya kuwa mhifadhi. Usitie shaka, jopo letu la washindi wa Tuzo la Whitley wana vidokezo vingi kwa ajili yetu!

"Unahitaji kuzungumza kutoka moyoni na wafadhili wanapenda kusikia hadithi za kweli kutoka ardhini. Kwa hivyo nilijifunza kwamba unapaswa kuwaacha wawe marafiki zako, sio wafadhili wako tu. Washirikishe katika safari mpaka utimizo. Ni ngumu kufanya wakati msingi wako wa wafadhili ni mkubwa sana lakini inafaa kukumbuka kila wakati." - Hotlin Ompusunggu



Kuchangisha pesa ni kipengele muhimu cha mradi wowote wa uhifadhi lakini inaweza kuonekana kama ulimwengu wa ajabu ikiwa hukuhitaji kuchangisha pesa hapo awali. Rodrigo Medellín amekuwa akifanya hivyo kwa muda sasa na anasisitiza hitaji la kujiamini. Anasema: "Unapaswa kujihusisha, na unapaswa kuwa na hakika kabisa kwamba hii ndiyo hasa unayotaka kufanya".

Kutunga kazi yako vizuri pia husaidia kulingana na Laury Cullen. Kuwa mhifadhi katika Msitu wa Atlantiki kunamaanisha kupachikwa katika mojawapo ya mifumo ya ikolojia inayotishiwa zaidi kwenye sayari. Lakini pia anaweza kuiweka kama kesi ya lazima kwa uhifadhi, nyumbani kwa spishi za haiba kama vile tamarini za simba weusi na jaguar. Anaamini kuwa kufikiria kuhusu mazingira unayofanya kazi na jinsi unavyotaka kuiiza kwa wafadhili ni muhimu sana.

Ni njia gani bora ya kuuza kazi yako? Je, kuna aina fulani huko ambayo inaweza kukusaidia kupata ufadhili mahususi na hatimaye kukusaidia kulinda mfumo mzima wa ikolojia? Hoja hizo zote zinahitaji kuwa wazi katika kichwa chako kabla ya kwenda na kuzungumza na wafadhili watarajiwa.





Kuelewa matakwa na mahitaji ya wafadhili ni sehemu muhimu ya mchakato na jambo ambalo Caleb Ofori-Boateng anafahamu vyema. Anaeleza: "Labda natumia muda uleule, ikiwa si zaidi, kujaribu kuelewa mfadhili anayefaa kuliko kuandika pendekero la ufadhili. Ninasoma tovuti zao, nikiangalia vigezo vyao vya kustahiki, na kisha kutafuta watu ambao wamewafadhili hivi karibuni. Na haya yote kwa pamoja yameniweka katika hali ambayo ninaweza kufikiria kama mfadhili.

Ni muhimu pia kufikiria juu ya aina ya ufadhili tunayotaka kuingilia. Je, tunatarajia kupitia misingi ya kimataifa na kitaifa? Au tunatafuta michango ya kibinafsi? Elena Bykova anapendekeza kuangalia mashirika ambayo yanaweza kukuunganisha na wafadhili wanaoweza kukufadhili. Anaeleza: "Kuwa na uhusiano wa kipekee nao ni jambo zuri kwa sababu tunaweza kueleza kwa nini tunahitaji pesa hizo na jinsi zingeweza kuleta mabadiliko ya kimsingi. Inamaanisha pia kuwa tunaweza kujenga uhusiano wa muda mrefu na baadhi ya wafadhili wetu na wanakuwa marafiki zetu.



Purnima Barman akitoa ufhamu kuhusu korongo nchini India

Hoja hii iligusa washindi wengi wa Tuzo za Whitley walioangaziwa kwenye kijitabu hiki cha zana. Ni jambo moja kupata mfadhili lakini jingine kwa pamoja kujenga uhusiano huo na kuugeuza kuwa chanzo cha ufadhili wa muda mrefu. Laury anaongeza: "Mimi huwaalika wafadhili wetu wengi kuja kuona mradi huo. Ni kweli tunatumia ripoti na picha lakini hakuna kitu kinachofananishwa na kuja hapa na kukaa siku chache na wenyeji". Purnima Barman pia anaamini kuwa kuwa mwaminifu ni muhimu ili kudumisha uhusiano. Anasema: "Wanapaswa kujuu kinachoendelea kwa hivyo usione haya kwa kuwaeleza baadhi ya changamoto unazozipitia".



Ni muhimu pia kukumbuka kuwa wafadhili sio vyombo visivyo na uso. Amanda Vincent anatukumbusha kwamba tunataka kuwavutia kama watu. Anaeleza hivi: "Unataka kuwafanya watu hao wajivunie na unataka kuwafanya watu hao wahisi kwamba umehusika kikamilifu. Kwa hivyo andika ripoti zako kwa wakati unaofaa na ufanye bidii kujaribu kuungana na wafadhili kupitia njia zingine za mawasiliano".

Mwisho, miradi ya uhifadhi mara nyingi hutuhitaji tuweze kubadilika na kunyumbulika katika jinsi tunavyoiendeza 12 kwa hivyo Shivani Bhalla anapendekeza vyanzo vya ufadhili wa aina mbalimbali iwezekanavyo badala ya kuweka mayai yetu yote kwenye kapu moja. Pia anatukumbusha kuwa uchangishaji pesa sio lazima ufanywe na mtu mmoja: "Zungumza na timu yako! Nadhani hiyo ni kidokezo muhimu kwa mtu yeyote ambaye anahisi kwamba shinikizo zote ni juu yake kuchangisha pesa. Ni muhimu kuangalia karibu na timu yako na kuuliza ikiwa kuna mtu mwingine yeyote anayetaka kuchangisha pesa. Kisha unaweza kumsaidia na kumfundisha mtu huyo."

"Ni jambo liliosemwa sana, lakini uvumilivu ni muhimu na unahitaji tu kuendelea kutuma ombi." - Çağan Sekercioğlu





VIDOKEZO VYA KUANZA

Je! una nia ya kuanza baada ya kusoma ushauri huu wote? Hapa kuna vidokezo vitano ambavyo washindi wa Tuzo la Whitley walituambia wangetamani wangevijua walipoanza kazi yao!



"Kitu pekee ambacho hakikubaliki ni kuendelea kuishi bila kufanya mabadiliko yoyote katika maisha yako mwenyewe." - Rodrigo Medellín

"Anza kuokoa bioanuwai nyumbani kwako mwenyewe kisha uunde cheche. Lazima uanze safari ya elimu ya mazingira nyumbani kwako mwenyewe."
- Purnima Barman



"Unaweza kuunda niche yako ambapo unafaa kabisa, na kisha unaweza kuzoea. Unaweza kuchangia ulimwengu kwa namna yoyote unayotaka" - Pablo Borboroglu



"Jifunze kuhusu sosholojia, ufundishaji, saikolojia, na hata isimu kwa sababu ni muhimu sana kuwa na ujuzi fulani kuhusu lugha tofauti. Kuwa na ujuzi na maarifa mbalimbali ni muhimu sana kufanya kazi kama mhifadhi." - Elena Bykova



"Kujifunza kunatokana na uzoefu nyanjani! Inakuja na kufanya kazi na watu na kupima na kujaribu vitu."
- Laury Cullen





WACHANGIAJI

1 Mexico
Rodrigo Medellín

2 Guatemala
Marleny Rosales-Meda

3 Brazil
Laury Cullen

4 Argentina
Pablo Borboroglu

5 Turkey
Çağan Şekercioğlu

6 Ghana
Caleb Ofori-Boateng

7 Kenya
Dino J. Martins
Shivani Bhalla

8 Uganda
Gladys Kalema-Zikusoka

9 Indonesia
Hotlin Ompusunggu

10 Philippines
Amanda Vincent

11 India
Purnima Barman

12 Uzbekistan
Elena Bykova



Purnima Barman, wa shirika lisilo la kiserikali la Aaranyak, anachanganya uhifadhi wa korongo mfuko-shingo na mageuzi ya kijamii huko Assam - kutoa fursa za kiuchumi kwa zaidi ya wanawake 10,000 kwa kufuma motifu za korongo wa hargila katika mavazi ya kitamaduni. Alishinda Tuzo la Whitley mnamo 2017 na Continuation Award mnamo 2019.



Shivani Bhalla na shirika lake lisilo la kiserekali, Ewaso Lions, anafanya kazi na vijana-shujaa wa Samburu kumaliza mzozo kati ya wafugaji na wanyama wanaokula nyama nchini Kenya. Shivani alishinda Tuzo la Whitley la 2014 na kuongeza kazi yake na Ufadhilli wa Kuendelea (Continuation Award) wa 2016 na 2019.



Pablo Borboroglu alishinda tuzo la juu zaidi la WFN mnamo 2018 - Tuzo la Dhahabu la Whitley. Mwanzilishi wa Global Penguin Society, Pablo anachanganya sayansi, usimamizi na elimu ili kuhifadhi pengwini kote katika Ulimwengu wa Kusini, akiwatumia kama spishi kuu kwa uhifadhi mpana wa mazingira ya baharini.



Elena Bykova, kwa msaada wa Tuzo la Whitley la 2011 na Continuation Award ya 2013, ameokoa swala wa Saiga walio hatarini ya kutweka, kutokana na uwezekano wa kutweka kwenye nyanda za juu za Ustyurt nchini Uzbekistan. Sasa, baada ya kushinda Continuation Award ya 2020, yeye na timu yake katika Muungano wa Uhifadhi wa Saiga (Saiga Conservation Alliance) wanachukua mbinu kamili ya kurejesha mfumo wa kijamii nakiikolojia katika Bonde la Bahari ya Aral.



Çağan Hakkı Şekercioğlu ni kikosi kinachoongoza kwa uhifadhi nchini Uturuki. Kwa ushinda wao wa Tuzo la Dhahabu la Whitley la 2013 na raundi kadhaa za Continuation Award, yeye na Shirika lisilo la kiserekali, KuzeyDoğa, kwa sasa wanafanya kazi ya kulinda mifumo ya ikolojia ya ardhioevu huku ikileta manufaa halisi kwa wenyeji.



Laury Cullen, akiwa ameshinda Tuzo la Whitley la 2002 na raundi tano zilizofuata za Continuation Award, amekuwa kiongozi wa ulimwengu katika suluhisho zinazotegemea asili kwa mabadiliko ya hali ya hewa. Akiwa na shirika lisilo la kiserekali, IPÊ, amerejesha ukanda mkubwa zaidi wa msitu wa Brazili wenye miti milioni 1.4 iliyokuzwa katika vitalu vya jamii. Pamoja na kupunguza kaboni na kusaidia familia za vijijini, kazi hii inaunganisha tena wanyamapori waliotengwa ikiwa ni pamoja na tamarin simba weusi (black lion tamarin), jaguar na tapir.



Dino J. Martins amefanya utafiti mahusiano ya mimea na wadudu, akashirikiana na wakulima katika kilimo endelevu, na kuchangia kwa sheria ya serikali ya Kenya dhidi ya dawa za kuua wadudu. Kujitolea kwake kwa maisha yote katika wasafilishaji poleni na watu kunaboresha usalama wa chakula, na kuimarisha maisha na kuhifadhi viumbe hai kote Afrika Mashariki. Kwa kushinda Tuzo ya Dhahabu ya Whitley ya 2015, yeye ndiye mhitimu wa kwanza kuijunga na Bodi ya Wadhamini ya WFN.



Rodrigo Medellín - Mwana Popo wa Mexico - ameungwa mkono na WFN kwa miaka 17, ambapo amepanua kazi yake hadi nchi 16 katika mabara 4. Akiwa na shirika lisilo la serikali, BIOCONCIENCIA, amefanya kazi muhimu na inayopimika kwa kubadilisha jinsi watu wanavyowachukulia popo, akikuza umuhimu wao kwa kusambaza poleni, udhibiti wa wadudu na usambazaji wa mbegu.



Caleb Ofori-Boateng alishinda tuzo la 2019 la Whitley. Caleb ambaye ni daktari wa reptilia na amfibie wa kwanza wa Ghana aliyefunzwa kirasmi, alimgundua na sasa anamlinda chura anayeteleza wa Togo katika shirika lake lisilo la kiserekali, Herp Conservation Ghana.



Hotlin Ompusunggu alipokea tuzo la 2011 la Whitley, Tuzo la Dhahabu la Whitley la 2016 na bado anazidi kutia juhudi na Ufadhilli wa Kuendelea wa 2019 (2019 Continuation Funding). Umaskini na afya duni ni vichochezi vya ukataji miti nchini Indonesia kwa hivyo Hotlin na shirika lake lisilo la kiserikali, Healthy Planet Indonesia, wanatoa huduma ya afya bila malipo nawao wanaofaidi wapande miti katika makazi muhimu ya orangutan.




Marleny Rosales-Meda anahakikisha kuwa ujuzi asilia wa uwindaji endelevu unaarifu uhifadhi wa mazingira na sheria za kitaifa nchini Guatemala. Kwa ushindi wake wa Tuzo la Whitley la 2008 na kushindi awamu tatu za Continuation Award ili kusaidia uundaji wa eneo la kwanza la uwindaji lililoidhinishwa kisayansi na wanajamii, anafanya kazi na Shilika lake lisilo la kiserikali, ORCONDECO, kujenga uwezo wa uhifadhi kupitia uongozi wa vijana.



Amanda Vincent alishinda tuzo la kwanza kabisa ya Whitley! Kwa zaidi ya miaka 30 ameangazia biashara ya mbuzi-bahari (seahorse) nchini Ufilipino, amekabiliana na mazoea haribifu ya uvuvi kama vile uvuvi wa chini ya bahari na akashawishi usimamizi endelevu wa baharini na sera kupitia kwa shirika lake lisilo la kiserekali, Project Seahorse.



Gladys Kalema-Zikusoka inalinda afya ya sokwe wa milimani na watu ambao wanatumia kwa pamoja nafasi, rasilimali na 98% ya Asidi nasaba (DNA) zao. Alikuwa daktari wa kwanza wa wanyamapori nchini Uganda kabla ya kuanzisha Hifadhi ya Kupitia Afya ya Umma na (Conservation Through Public Health), na tangu kushinda Tuzo lake la Dhahabu ya Whitley ya 2009 na Continuation Funding, amekuwa mhifadhi anayetambulika kimataifa.



Shukrani kwa:

DHANA NA MUUNDO WA JUMLA

Julia Migné aliye changia kwa dhana na maudhui na.

The Whitley Award winners were interviewed by Giada Giacomini, Iona Cunningham-Eurich, Julia Migné, Sarah Wheedleton, Sofia Castelló y Tickell, Susana Veloso Soares, Trisha Gupta, and Will Sharkey.

Maelelezo yalikusanya na Maria Carbin.

Washindi wa Tuzo za Whitley walihojiwa na Giada Giacomini, Iona Cunningham-Eurich, Julia Migné, Sarah Wheedleton, Sofia Castelló y Tickell, Susana Veloso Soares, Trisha Gupta, na Will Sharkey.

Kimetafsiriwa kwa Kiswahili na: Consolata Gathoni Gitau na Alice Karuri.

Picha: Carla Rhodes (picha ya Purnima Barman uk.25), HJ Koldewey (picha ya Amanda Vincent uk.26), Les Films au Clair de Lune (picha ya Caleb Ofori-Boateng uk.26), Nina Fascione (picha ya Shivani Bhalla p.25), Stacey Iverson (picha ya Elena Bykova uk.25).

MFADHILI

Whitley Fund for Nature

**KILICAPISHWA KWA MARA YA KWANZA NCHINI
UINGEREZA MNAMO MWAKA WA 2022 NA CONSERVATION
OPTIMISM**

Zana hii imeidhinishwa chini ya Leseni ya Kimataifa ya Creative Commons Attribution-ShareAlike 4.0.

Tunahimiza utoaji wa Kijitabu vingine wa aina zote, kwa njia zote za kielektroniki, ufundu, kurekodi au vinginevyo.

LULU ZA BUSARA KWA WAHIFADHI **CHIPUKIZI**



SUPPORTING
CONSERVATION
LEADERS

